MWITO PROGRAM KISWAHILI SCRIPT

PROGRAM NUMBER 1141

SCRIPTURE:ROMANS 8 :18

DURATION:15 MINUTES.

Ni furaha kuu kukukaribisha kwenye kipindi cha Mwito ambacho hukujia saa na wakati kama huu kupitia idhaa ii hii.Ilivyo kawaida ya kipindi hiki ni kukuelimisha na kukujumuisha katika kundi la wale walio na hamu ya kueneza injili ya wokovu ya Yesu Kristo.Kaa tayari manake mwishoni mwa kipindi hiki nitakupatia simu ya mawasiliano na jinsi unavyoweza kujipatia agano jipya la Bibilia takatifu.Kwa mara nyingine tena nakukumbusha kuwa kipindi hiki kinakujia kwa hisani na ufadhili wa huduma ya kimataifa ya Macedonian Call yake mchungaji Harold Williams.Tunashukuru huduma hiyo na wengine ambao wamejitolea kuhakikisha kuwa unapokea mfululizo wa vipindi hivi kwa gharama yao.Kumbuka rafiki yangu gharama ya kununua muda wa kurushia vipindi hivi ni kubwa,ndiposa twawapa shukrani wafadhili wetu.Nakukumbusha ndugu msikilizaji kwamba kipindi hiki ni nambari 1141.

Somo lililopita tulikamilisha kwa kuchambua aya za 16 na 17 zilizosema hivi na 17..***Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu ya***

kuwa sisi tu watoto wa Mungu na kama tu watoto,basi tu warithi;warithi wa Mungu,warithio pamoja na Kristo;naam tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye

Naam mskilizaji wangu nasema karibu kwa ajili ya somo la leo.

Ningependa kabla ya kuzama kabisa kwenye somo letu ,tuangazie kwanza aya ya 18 ambayo itatupatia himizo kuu…***Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu.Kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu.***

Bila shaka msikilizaji wangu ahadi hiyo ni mojawapo muhimu sana na ya kutia moyo katika bibilia.Inawapa tumaini wale wanaoteseka ama kupitia mikono ya binadamu au matukio ya kawaida ya kila siku.Labda ni mateso kutokana na magonjwa au hisia kutokana na huduma kwa Bwana wetu Yesu Kristo.Na ningependa kukufahamisha kuwa hata wakati huu ninaposhiriki nawe kwenye kipindi hiki,kunao wamishenari ambao wanapitia ugumu fulani wa kihisia au maudhi yanatokana na kufanya kazi katika mazingira tofauti ya kitamaduni tofauti na ya kwao.Na sio hayo tu bali pia wanateseka kutokana na ugumu wa kuishi katika mazingira hayo.Kunao wale ambao wanahudumu kwenye nchi za ukanda wa joto na magonjwa ambayo si rahisi kutibika.

Ningependa hata hiyo nikufahamishe kwamba sio lazima tuende kuhudumu katika nchi za kigeni au mazingira ya mbali ndipo tukumbane

na hali hizi.Pia wahudumu wa neno la Mungu wanakabiliana na pingamizi kutoka familia zao au jami zao.Kunazo pingamizi za moja kwa moja dhidi ya neno la Mungu.Kumbuka kuna wale ambao wao pekee yao ndio wameokoka katika familia zao na wakapata ukinzani mkali kutoka kwa ndani.Wao ni kama taa inayoangaza kwenye kiza totoro.Wao ni kama chumvi ambayo imepakwa kwenye kidonda kwa kusudi ya kukiponya.Neno moja la busara lililonenwa kwa hekima hutuliza fujo.Najua siku ya leo ninanena na mamilioni ya watu kupitia redio katika sehemu tofauti za ulimwengu.Ningependa wafahamu kuwa Mungu anayaelewa na kuyajali mateso wanayopitia.Iwe ni mateso au maumivu kutokana n ajali au mateso Mungu anayaelewa na hajakusahau.Kwa wakati na majira yake atakufikia na kukuokoa kutoka hali hiyo.

Lakini ni kwa ni haya yote hutokea.Ni kwa sababu ya ukosefu wa imani? La hasha! Naam kuna sababu lukuki kuhusiana na swali hilo.Kuna nyakati tunatumbukia katika hali hiyo kutokana na sababu za ubinafsi wetu.Kuna wakati tunajiingiza kwenye mitego ya mateso kutokana na hisia zetu na hali ya shingo ngumu.Lakini kumbuka mwenzangu msitari usemao yote hufanyika kwa wema kwa wale wampendao Bwana na ambao wameitwa kwa kusudi lake.Nadhani ni warumi sura ya 8:28.Kwa wale ambao mnaendelea kupata nafuu nyumbani kwenu ,wale walio hospitalini,kwa wakongwe ambao wamepita muda wao wa ujana na sasa wanakabiliwa na changamoto za kiafya,hebu niseme huo ni mwelekeo wa kimaumbile.Waingereza wanasema ***Natural progression***.Ni hali

nayotarajiwa madamu tuko hai na tutaishi hadi umri mpevu.Bibilia inasema tulikuja ulimwengu huu tukiwa wenye dhambi;tukizungumza uwongo tukiwa na tabia ya ubinafsi na kwamba kiasilia sisi ni wenye dhambi tu.Tulianza kutenda dhambi hadi tulipofikia umri wa uwajibikaji,ambapo tulianza kuchagua kutenda dhambi au kuepukana nazo.Na tumefikia wakati ambapo dhambi imeathiri pakubwa maisha yetu na kutuacha na makovu mabaya.Na tunapozeeka athari za dhambi hujitokeza kwenye miili yetu.Na ningependa nikuhakikisie mpendwa isipokuwa Henoko na Eliya,ambao hawakuonja mauti,hatutakosa kupitia hayo yote au laba Yesu arudi tungali katika miili hii ya kibinadamu.Mimi binafsi naitamani siku hiyo na jinsi Yohana alivyosema natamani kuwadia siku hiyo.Lakini ikiwa Yesu atarudi kabla ya hapo,basi letu ni kujiweka tayari.

Ikiwa ulikuwa nasi tulipoanza kuchambua aina mbili za asili ya mwanadamu katika sura za 6 na 7 za Warumi,bila shaka utakumbuka kuwa kuliikuwa na yule mtu wa kale aliyeathiriwa na dhamb na mtu wa pili ambaye ameokolewa.Ule utu upya.Usisahau kuwa yule mtu wa kale yungali anatuandama hata tunapokusudia kutenda mema.Waweza kwa umeokolewa na kusamehewa dhambi zako ,lakini ule utu wa kale ungali unakusumbua.Na huo utu wa kale natuathiri hata na afya zetu hadi uzeeni.Hata hivyo tusisahau kwamba Mungu hutumia fursa hiyo kutufinyanga upya hadi kufikia umbo analolitaka.Malaki anatukumbusha kuhudsu ile taji atakayoivalia Munu.Taji iliorembwa kwa lulu za thamani

na sisi ndio zile lulu zinazotayarishwa.Na siku ile tutakapodhihirishwa,tutadhihirishwa kama lulu za Mungu wetu mkuu.Kumbuka almasi hutokana na utaratibu mrefu sana na mbinyo wa miaka mingi wa ardhi na joto kubwa.Na hilo joto na mbinyo ndio anaoutumia Munu kutuandaa kwa ajili ya siku hiyo.

Nasikitika msikilizaji sitaendelea na uchambui huo kwa sasa kwa kuwa muda wangu umeniiishia.Lakini ningependa kuuuliza ikiwa uko tayari kmpokea Kristo arudipo kuwachukua walio wake? Umechagua kumtumikia Mungu kuitia mwanawe Yesu Kristo? Kwa ufupi ,umeokoka? Ikiwa bado chukua hatua.Nakupatia fursa hii ikiwa hujampokea Kristo kuwa mwokozi wako ,ufanye hivyo.Sema ombi hili fui nyuma yangu kisha nitakwelekeza hatua nyingine za kuchukua…. ***Bwana Yesu,naja kwako nilivyo.Nimetambua nimekuwa nikiishi maisha ya dhambi .Lakini sasa ninatubu.Nisamehe dhambi zangu na unifanye kiumbe kipya.Ingia ndani ya maisha yangu na kwa roho wako mtakatifu unitakase na kunifanya kiumbe kipya,kwa utukufu wa jina lako.katika jina la yesu Kristo nimeomba na kuamini .Amina.***

Ikiwa umeomba ombi hilo fupi ukimaanisha nakuhakikisha kuwa umeokoka kwa mujibu wa imani yako.Sasa chukua hatua ya kutafuta kikundi au kanisa litakalokusaidia kuweka msingi imara wa wokovu.Ikiwa unashiriki katika kanisa linloamini wokovu,jitambulishe kwa uongozi ili ukusaidie kuweka msingi wa wokovu wako.

Nitafurahi ikiwa utwasiliana nasi ili kuweze kukupatia vijitabu vya kukusaidia kwenye njia hii ya wokovu.. Zaidi ya hayo.Nitafurahi sana nitakapopokea maoni yako kukihusu kipindi hiki na hasa jinsi ya kukifanya kiwe cha manufaa zaidi kwako.Hiki kimekuwa kipindi cha Mwito nambari 1141.Naomba uwasiliane nami kupitia njia ya arafa ukitumia nambari ifwatayo-: **0721 970 520**. Au 020 2679842.Ikiwa unaishi Nairobi tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive,off Ngong Road, baada ya jumba la TOP PLAZA.Anwani yangu ikiwa utaniandikia barua ni-:Kwa mtayarishi,Mwito,S.L.P.21514-00505 Nairobi.Waweza pia kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatavyo-barua@twr.co.ke.Na basi kufikia hapo sina budi kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu kutoka kwake Mungu wetu mtukuka.Juma lijalo tutaendelea kuijadili aya iyo hiyo ya 18 ya sura ya 8 ya kitabu cha Warumi.Ni mwaandazi wa kipindi hiki ndugu Charles Otunga ninayekuaga nikikutakia mbawazi zake Mungu wetu asiyelinganishwa na mwingine.**Kwaheri.**